Name ..... Adm No..... Class..... No..... Sign .....

NYABURURU GIRLS' NATIONAL SCHOOL

OUR LADY OF LOURDES

Tarehe	
Msimamizi	
Kurejeshwa	
Kudurusu	

KIDATO CHA KWANZA

TATHMINI YA TATU

MUHULA WA PILI 2016

MUDA: MASAA MAWILI

Maagizo

- Yajibu maswali yote.
- Majibu yote yaandikwe kwa nafasi zilizoachwa.

Www.Manyanfranchise.Com

SEHEMU	ALAMA	
INSHA	20	
UFAHAMU	20	
SARUFI	50	
FASIHI SIMULIZI	10	
JUMLA	**100**	

Name ..... Adm No..... Class..... No..... Sign .....

SEHEMU A: INSHA (ALAMA 20)

Andika onyo lolote linalopatikana katika mazingira ya shule.

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

www.Manyamfranchise.Com

Name ..... Adm No..... Class..... No..... Sign .....

.....

.....

SEHEMU B: UFAHAMU (ALAMA 20)

Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali yanayofuatia

CHANZO CHA UTOVU WA NIDHAMU SHULENI

Shule inaweza kuwa na **nidhamu** ya hali ya juu kutegemea uongozi uliopo. Hata hivyo, iwapo wanafunzi wanajua vizuri udhaifu uluioko kwa viongozi basi wanaweza kutumia fursa hiyo kuimarisha nyendo zao zisizofaa.

Kwa mfano wanafunzi wakijua wanaweza kumdanganya mwalimu mkuu na kupata ruhusa kutoka nje, basi waweza kutumia fursa hii kuingiza vileo kama pombe na dawa za kulevya shuleni.

Utovu wa nidhamu hujitokeza katika sura mbalimbali. Baadhi ya mambo haya yakionekana shuleni basi mwalimu mkuu na kundi lake wakaze juhudi zao kwa maana kuna tatizo.

Mwanafunzi asiye na haja na masomo hatajisumbua kufanya kazi ya mwalimu. Hii ni kwa sababu hayapi masomo yake umuhimu na kuyaona kama jambo la pekee lililompeleka shuleni. Migomo ya mara kwa mara ya wanafunzi haionyeshi kuwa wanafunzi wamenyimwa haki zao, lakini inaonyesha kuna utovu wa nidhamu.

Kwa kawaida kama wanafunzi wakitaka kufanyiwa jambo, huwatuma **viranja** wao au **walimu wao wa madarasa**. Lakini pale ambapo wanafunzi hawasemi lolote mchama, ila wanangojea giza ili waimbe "**nyimbo za ukombozi**", basi pana tatizo. Kila shule huwa na namna yake ya kuwasiliana kati ya wanafunzi na uongozi. Njia hii yafaa iheshimiwe ili kuleta uelewano kati ya wanafunzi na walimu.

Wanafunzi pia wataonyesha utovu wa nidhamu iwapo hawatekelezi majukumu yao mengine. Kwa mfano: kusafisha darasa, bweni, **maktaba** au **maabara**. Mwanafunzi mwenye nidhamu hahitaji kusukumwa ili kutekeleza majukumu yake. Hufanya kwa wakati unaofaa na pia huyafanya vizuri na kwa ukamilifu. Hivyo iwapo mwanafunzi ni lazima akumbushwe majukumu yake na asukumwe au asimamiwe kuyafanya, basi kuna tatizo.

Visa kama vile uvutaji na ulevi ni visa vibaya sana na ambavyo vinahitaji kushughulikiwa haraka. Visa hivi vikiwa vingi basi vinaashiria utovu wa nidhamu ambao bila shaka unaporomosha masomo. Visa hivi pia ikumbukwe vinaambukizwa kama ugonjwa na vikiachwa basi vinaweza kuwa mtindo wa maisha katika shule nzima.

Kupigana kukiripotiwa shuleni na tena iwe kwamba visa hivi vinazidi, basi hii ni ishara kuwa wanafunzi hawana njia nyingine ya kutatua mizozo yao isipokuwa kupigana. Visa hivi pia

www.Manyamiranchise.com

vinaashiria utovu wa nidhamu miongoni mwa wanafunzi. Vinaonyesha kuwa tofauti zozote zile hazitatuliwa kwa mazungumzo ila kwa masumbwi.

Kadhalika iwapo wanafunzi wa vidato vingine wanawaadhibu sana wanafunzi wa kidato cha kwanza, basi huu ni utovu wa nidhamu. Wanafunzi hawa huandhibiwa badala ya kukaribishwa. Ajabu gani hii! Miongoni mwa mambo wanayofanywa ni kuchapwa, kunyang'anywa chakula, kufanywa wawaoshee wenigne nguo na wawatekelezee majukumu yao. Katika harakati hizi wengine hata hulazimishwa kunywa na kutumia vileo ili wakubalike katika makundi ya wakubwa wao. Visa hivi humwathiri mwanafunzi kisaikologia.

Mgeni akija angalau hupewa chai ndipo siku ya pili apewe jembe akalime. Wanafunzi wengi wa kidato cha kwanza hawapati kufurahia kuupasi mtihani wao wa darasa la nane. Badala yake wakijiunga na shule nyingine hujipata wakijuta kuupasi mtihani.

Visa vya wanafunzi wengine kuacha shule kwa sababu ya **masaibu** haya vimeripotiwa. Visa vingine huwa viovu hivi kwamba humwathiri mwanafunzi siku zake za baadaye.

Dawa za kulevya huchangia pakubwa sana katika utovu wa nidhamu. Dawa humtoa mtumiaji kutoka kwa ulimwengu huu na kumtia katika ulimwengu wake mwenyewe. Elimu na maisha kwa jumla hupoteza maana akataka kumtumikia "**kiongozi wake**", yaani dawa. Tena kwa sababu ya kuyainda usiku na kulala mchana, basi mwanafunzi hawezi kufanya vyema masomoni.

(Makala haya yamenukuliwa kutoka *Taifa Leo*, Mei 3, 2004)

Www.Manyamfranchise.Com

Maswali

(a) Nidhamu shuleni hutegemea nini? (al.3)

.....

.....

.....

.....

.....

(b) Je, ni kweli kwamba migomo huashiria kwamba wamenyimwa haki zao? Eleza. (al.2)

.....

.....

.....

.....

....

(c) Taja sifa nne za mwanafunzi mwenye nidhamu. (al.4)

.....

.....

.....
.....
.....
.....

(d) Taja athari nne za dawa za kulevya kwa mwanafunzi. (al.4)

.....
.....
.....
.....
.....

(e) Toa maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika makala haya: (al 5)

(i) Nidhamu.....

(ii) Udhaifu.....

(iii) Viranja.....

(iv) Nyimbo za ukombozi .....

(v) Maktaba .....

(f) Andika kichwa kingine cha taarifa uliyoisoma. (al 2

.....

www.Manyamfranchise.com

SARUFI

(a) Taja sauti mbili mbili ambazo ni:

(i) Vipasuo _____ _____ (al.2)

(ii) Nazali _____ _____ (al.2)

(b) Andika ngeli za nomino hizi:

Name ..... Adm No..... Class..... No..... Sign .....

(i) Bustani..... (al.2)

(ii) Ndimi ..... (al.2)

(iii) Manukato ..... (al.2)

(iv) Kipepeo ..... (al.2)

(c) Tambulisha aina za maneno katika sentensi ifuatayo. (al.4)

Jamani! Msaidieni ajuza huyo.

.....

(d) Onyesha viambishi awali na tamati katika: (al.4)

(i) Watatukaribisha

(ii) Uliotatizika

(e) Eleza maana mbili zinazojitokeza katika sentensi hii: (al.4)

Alimpigia mpira

.....

.....

.....

.....

(f) Kanusha sentensi hizi:

(i) Tuliimba tukavuna mahindi (al.2)

.....

www.Manyamfranchise.Com

(ii) Maharawe yalivunwa na kutiwa ghalani (al.2)

.....

.

(g) Andika sentensi ziufatazo upya ukizingatia maagizo yaliyo kwenye mabano.

(i) Mazingira yamehifadhiwa (Hali ya mazoea) (al.2)

.....

(ii) Mwalimu anasahihisha kitabu cha mwanafunzi. (Anza kwa: Kitabu..) (al.2)

.....

.....

(h) Tunga sentensi zenye miundo hii na uionyeshe waziwazi. (al.4)

(i) KN + KT(kundi nomini na kundi tenzi)

.....

.....

.....

(i) Andika sentensi zifuatazo bila ya kutumia kirejeshi amba-

(i) Fulani ambayo imefumwa ni nyekundu (al.2)

.....

(ii) Matendegu ambayo yametengenezwa ni ya kitanda ambacho kilivunjika juzi (al.2)

.....

.

(j) Andika katika hali ya kufanywa. (al6)

i. Taa zilizimika ghafla

.....

ii. Mtoto alivibeba vikapu ghafla.

.....

iii. Punda wa mkulima amekufa.

www.Mahyanfranchise.Com

Name ..... Adm No..... Class..... No..... Sign .....

.....
.....

(k) Andika katika wingi. (al4)

i. Waondoe watoto wale karibu na makaa ya moto.

.....
.....

ii. Maduka yauzayo bidhaa uzitakazo yamefungwa

.....
.....
.....

FASIHI SIMULIZI

Eleza majukumu matano ya fasihi katika jamii (al.10)

.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....

Www.Manyamfranchise.Com